JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe:
rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JUNI 29, 2020

TAKUKURU MKOA WA ARUSHA INAWASHIKILIA WATU TISA WAKIWEMO VIONGOZI WA JUMUIYA YA WAZAZI YA CCM KWA MAKOSA MBALIMBALI YA RUSHWA

TAKUKURU Mkoani Arusha katika nyakati na matukio tofauti imewakamata na kuwashikilia jumla ya watu tisa ambao ni viongozi wa Chama, watumishi na wafanyabiashara kwa makosa mbalimbali ya rushwa. Watu hao wanaao shikiliwa ni :

1. SIFAEL SIYALOI PALLANGYO – MJUMBE WA BARAZA LA JUMUIYA YA WAZAZI(M) ARUSHA

2. UPENDO MALULU NDOROS – KATIBU WA MALEZI (W) LONGIDO NA MJUMBE WA BARAZA LA WAZAZI (M) ARUSHA.

3. LARAPOSHO KATEWA LAIZER – KATIBU WA WAZAZI (W) LONGIDO/MJUMBE WA BARAZA LA WAZAZI (M) ARUSHA.

4. GODWAIT CHARLES MUNGURE – KATIBU WA WAZAZI KATA YA KIKATITI MERU.
5. MBOIYO NAISIKIE MOLLEL – AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA TUKUSI KATA LOLKISALE WILAYA YAMONDULI

6. MIKIDADI ZAKARIA MOLLEL – MWENYEKITI WA KAMATI YA PEMBEJEO KIJIJI CHA TUKUSI KATA LOLKISALE WILAYA YA MONDULI

7. KANANKIRA JACKSON NNYARY – WAKALA WA PEMBEJEO ZA KILIMO KIJIJI CHA LOITA KATA YA NKOANRUA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

8. GERVAS ANDREA MOLLEL – MFANYABIASHARA WA KATA YA OLTRUMET WILAYANI ARUMERU, pamoja na

9. JOSEPH CHRISTOPHER MOLLEL - MFANYABIASHARA WA KATA YA OLTRUMET WILAYANI ARUMERU

Ufafanuzi wa Makosa:

Katika tukio la kwanza, TAKUKURU Mkoani Arusha mnamo Juni 26, 2020 ilipokea taarifa kutoka kwa Raia mwema kwamba Lilian Ntiro ambaye anatarajia kugombea Ubunge wa Viti Maalum (wazazi) Mkoa wa Arusha alikuwa amempatia SIFAEL SIYALOI PALLANGYO – Mjumbe wa Baraza la Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha fedha kwa ajili ya kwenda kuwahonga wajumbe wa Baraza la Wazazi katika Wilaya ya Longido kama kishawishi cha kumpigia kura katika kura za maoni zinazotarajia kufanyika hivi karibuni.

Baada ya kupokea taarifa hiyo TAKUKURU Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Longido waliandaa mtego na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa wanne kila mmoja akiwa na kiasi tofauti cha fedha zilizokuwa zimeandaliwa kugawiwa kwa wajumbe wa Baraza la Wazazi wilayani Longido. Watuhumiwa hao waliokamatwa ni; SIFAEL SIYALOI PALLANGYO – Mjumbe wa Baraza la Jumuiya ya wazazi (M) Arusha ambaye alikutwa na Sh 14,000/=, UPENDO MALULU NDOROS – Katibu wa Malezi (W) Longido/Mjumbe wa Baraza la Wazazi (M) Arusha ambaye alikutwa na Sh. 552,000/= pamoja na simu aina ya ITEL smart phone ambapo kulikuwa na mawasiliano baina yake na watuhumiwa wenzake, LARAPOSHO KATEWA LAIZER – Katibu wa Wazazi (W) Longido/Mjumbe wa Baraza la Wazazi (M) Arusha ambaye alikutwa na sh. 117,000/= pamoja na simu aina ya Samsung Galaxy ambapo kulikuwa na mawasiliano baina yake na watuhumiwa wenzake na GODWAIT CHARLES MUNGURE – Katibu wa Wazazi kata ya Kikatiti Meru ambaye, alikutwa na simu ndogo ikiwa na mawasiliano ya mara kwa mara na SIFAEL SIYALOI PALLANGYO. Uchunguzi wa tuhuma hii unaendelea. Watuhumiwa hao wako mahabusu tangu Juni 26, 2020 na wanarajiwa kupewa dhamana leo huku TAKUKURU ikiendelea kumshikilia Mtia Nia Lilian Ntiro kwa mahojiano.

Katika tukio la pili, TAKUKURU Mkoani Arusha inawashikilia watuhumiwa wawili ambao ni GERVAS ANDREA MOLLEL na JOSEPH CHRISTOPHER MOLLEL – wote wafanyabiashara wa Kata ya Oltrumet wilayani Arumeru kwa kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kiasi cha shilingi milioni kumi na tano (shilingi 15,000,000/=) kutoka kwa mfanyabiashara mwenzao Advera Kyaruzi mkazi wa Mto wa Mbu wilayani Monduli.

Awali ilielezwa kwamba wafanyabiasha hao wote walikuwa wakishirkiana katika kusafirisha mbegu za vitunguu kutoka Tanzania kwenda Uganda. Mnamo Septemba, 2018 baada ya kupakia mzigo ukiwemo wa Advera wenye thamani ya shilingi 15,000,000/= walikubaliana kuwa, Advera Kyaruzi, Gervas Andrea na Haruna Kitundu watangulie kwa basi kwenda mpaka wa Murongo ambako wangekutana na Joseph Christopher ambaye alikuwa ni dereva wa FUSO yenye namba T 449 ATT ambaye gari lake lilikuwa limebeba mzigo wa mbegu za vitunguu .Safari ilikuwa hivyo kama walivyokuwa wamepanga lakini walivyofika Mpakani, Gervas alisema anaumwa tumbo hivyo akampatia Advera kijana mwingine wa kuvuka nae mpakani. Advera alipojaribu kuwasiliana na Christopher ikawa hapatikani kwenye simu na hakuweza kumuona tena wala kupata mzigo. Tangu kipindi hicho Advera amekuwa akifuatilia fedha zake kutoka kwa watuhumiwa bila mafanikio.Watuhumiwa wako mahabusu na uchunguzi wa suala hili unaendelea.

Katika tukio la tatu, TAKUKURU Mkoani Arusha imewakamata watuhumiwa watatu ambao ni; MBOIYO NAISIKIEMOLLEL – Afisa Mtendaji wa kijiji cha Tukusi kata Lolkisale wilaya ya Monduli, MIKIDADI ZAKARIA MOLLEL – Mwenyekiti wa kamati ya pembejeo kijiji cha Tukusi kata Lolkisale wilaya ya Monduli na KANANKIRA JACKSON NNYARY – Wakala wa Pembejeo za Kilimo kijiji cha Loita kata ya Nkoanrua Halmashauri ya wilaya ya Meru, kwa kosa la Kughushi vocha za pembejeo za kilimo za ruzuku ambazo walitakiwa kuzigawa katika kijiji cha Tukusi kata ya Loikisale halmashauri ya wilaya ya Monduli mwaka 2016.

Ilielezwa kwamba watuhumiwa hawa walipaswa kugawa mbegu ya mahindi, mbolea ya kupandia na mbolea ya kukuzia kwa wakulima lakini wao waligawa mbegu tu na baadae katika vocha wakaonesha kuwa wamegawa vitu vyote hivyo jambo ambalo si kweli.

Uchunguzi wa tuhuma hii umekamilika na watuhumiwa wanatarajiwa kufikishwa Mahakamani leo tarehe 29 Juni, 2020.

Katika tukio jingine TAKUKURU Mkoani Arusha mnamo Juni 26, 2020 ilimfikisha Mahakamani Daniel Luka Mollel Mwenyekiti wa Kitongoji cha Olmotony halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya shilingi elfu sabini (shilingi 70,000/-) kutoka kwa Nai Joseph mkazi wa kitongoji cha Olmotony ili asimchukulie hatua, baada ya kubaini kwamba alikuwa amejiunganishia maji ya kijiji kinyume cha taratibu.

Awali na alieleza kwamba, alifika ofisi ya Mwenyekiti huyo mnamo Juni 21, 2020 kutaka kujua utaratibu wa kuunganishwa maji. Mwenyekiti huyo alimtaka kuandika barua ya maombi na kuambatanisha “CHAI” kwa maana ya fedha. Nai aliandika barua na kuipeleka lakini hakumkuta mwenyekiti na alivyorudi nyumbani alikuta mme wake ameunganisha maji. Baada ya mwenyekiti kubaini kwamba Nai amejiunganishia maji, alifika nyumbani kwake na kuanza kumtishia kumchukulia hatua za kisheria. Baadaye mwenyekiti huyo alimweleza kwamba iwapo anataka jambo hilo liishe aandike barua ya maombi na fedha kiasi cha shilingi laki moja (shilingi 100,000/=) na kumpelekea.

Taarifa hii ilipelekea kuandaliwa kwa mtego wa rushwa wa shilingi elfu sabini (shilingi 70,000/=) na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa mnamo Juni 25, 2020

kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15 (1) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawashukuru wananchi kwa kuiamini TAKUKURU na kuendelea kuipa ushirikiano kwa kutoa taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwenye Taasisi za Serikali na maeneo mengine. Hii inaashiria mwamko chanya wa wananchi katika kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawahamasisha wananchi kuendelea kutoa taarifa hasa katika kipindi hiki tunachoelekea kwenye maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kuwahakikishia kuwa taarifa zitakazopokelewa zitafanyiwa kazi kwa haraka na hatimaye kuwezesha kupatikana kwa viongozi wasiotoa rushwa ili kuchaguliwa.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Arusha inatumia fursa hii kuwaonya wale wote walioanza kuwarubuni wapiga kura kwa rushwa na kufanya kampeni kabla ya muda,kwamba vitendo hivyo wanavyovifanya ni kinyume cha Sheria na wakibainika watachukuliwa hatua kali.

Imetolewa na:

JAMES G. RUGE

…….
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA
……